**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

---

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

**24 APRILI, 2024**

## YALIYOMO

*Ukurasa*


**YALIYOMO** .......................................................................... i
**VIELELEZO** ..........................................................................iii
**VIFUPISHO VYA MANENO** .................................................. iv
**SEHEMU YA KWANZA**............................................................ 1
**1.0 UTANGULIZI**..................................................................... 1
1.1 Muundo wa Taarifa................................................. 1
**SEHEMU YA PILI** ......................................................................3
**2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**......3
2.1 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha mwaka wa fedha 2023/2024...................................................... 4
2.1.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara (Na. 6389) Mtumba, Dodoma............................................ 5
2.1.2 Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Lemugur (Na. 3175), Kisongo-Arusha........ 6
2.1.3 Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kujaza gesi asilia kwenye magari (CNG) (Na. 3162), Dar es Salaam ........................................................ 8
2.1.4 Mradi wa ujenzi bomba la kusafirisha gesi asilia kwa ajili ya kupikia na viwandani (Na. 3162), Mwenge-Mbezi Beach, Dar es Salaam . 11
2.1.5 Mradi wa Umeme Vijijini (REA) (Na. 3113) Halmashauri ya Chalinze, Bagamoyo, Mkoa wa Pwani ................................................................ 12
2.2Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ....................... 14
2.3Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2024........................................... 16
2.4Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2024............................................. 17
2.5Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ..................................... 20

**SEHEMU YA TATU** ........................................................ 22
**3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

3.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........................................ 22
3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........................................ 24
3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........................................ 25
3.4 Ulinganisho baina ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa ........................................ 27
3.5 Uchambuzi wa Masuala Mahsusi ........................ 29
3.5.1 Mwenendo wa Upatikanaji wa Umeme ..... 29
3.5.2 Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini.......... 32
**SEHEMU YA NNE** ........................................................ 34
**4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ..... 34
4.1 Wizara ya Nishati ........................................ 34
4.2 Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO) . 34
4.3 Wakala wa Umeme Vijijini –REA ........................ 36
4.4 Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC) ................ 37
4.5 Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli – PURA ........................................ 38
4.6 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ........................................ 39
4.7 Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) 40

**SEHEMU YA TANO** ........................................................ 42
**5.0 HITIMISHO** ........................................................ 42
5.1 Shukrani ........................................................ 42
5.2 Hoja ........................................................ 44

# VIELELEZO

**Kielelezo Na. 1**: Ulinganisho wa bei za nishati mbalimbali katika kupikia ........................................................................................... 12

**Kielelezo Na. 2:** Makusanyo ya Maduhuli hadi Februari, 202417

**Kielelezo Na. 3:** Upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa kipindi cha Julai, 2023 - Februari, 2024 ............... 19

**Kielelezo Na. 4:** Ulinganisho wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025.................................... 25

**Kielelezo Na. 5:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 ............................ 27

**Kielelezo Na. 6:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........... 29

**Kielelezo Na. 7:** Mchanganuo wa uwezo wa mitambo katika gridi ya Taifa hadi Mwezi Februari, 2024 .................. 30

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AfDB | African Development Bank |
| CNG | Compressed Natural Gas |
| EWURA | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| JNHPP | Julius Nyerere Hydropower Project |
| LNG | Liquified Natural Gas |
| LPG | Liquefied Petroleum Gas |
| MW | Megawatt |
| NHC | National Housing Corporation |
| OC | Other Charges |
| PAET | PanAfrican Energy Tanzania Ltd |
| PBPA | Petroleum Bulk Procurement Agency |
| PE | Personal Emolument |
| PURA | Petroleum Upstream Regulatory Authority |
| REA | Rural Energy Agency |
| SCADA | Supervisory Control and Data Acquisition |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company Limited |
| TANOIL | TANOIL Investment Limited |
| TBA | Tanzania Building Agency |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TIPPER | Tanzania International Petroleum Reserves Limited |
| TPDC | Tanzania Petroleum Development Corporation |

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Nishati **(Fungu 58)** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025**.** Uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na maoni ya kamati kuhusu bajeti ya mwaka 2024/2025 ni kutokana na majukumu ya msingi iliyopewa Kamati kwa mujibu wa kanuni ya 117(2) ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[2].

## 1.1 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge,

---

[1] 118 (9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu zifuatazo:

a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, msingi na muundo wa taarifa hii;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, inaweka masharti kwa Kamati za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata[3]. Kwa kuzingatia matakwa haya, kuanzia tarehe 20 hadi 28 Machi, 2024 Kamati ilitekeleza wajibu huo kwa kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho dhidi ya mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilijielekeza kwenye maeneo yafuatayo: -

(a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

[3] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata

(c) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(d) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2024; na

(e) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati;

## 2.1 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge[4], inaweka masharti kwa Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2023/2024). Katika kuzingatia masharti hayo, Kamati ilifanya ziara katika mikoa minne ambayo ni Dodoma, Arusha, Dar es Salaam na Pwani na kukagua miradi minne (4) inayotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati.

Lengo la ukaguzi huo ni kutathmini utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kubainisha mafanikio na changamoto ili kuweza kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua katika kuisimamia Serikali. Uchambuzi kuhusu miradi hiyo na matokeo ya ukaguzi ni kama ifuatavyo: -

[4] Toleo la Februari 2023

### 2.1.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara (Na. 6389) Mtumba, Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) kwa ajili ya ofisi za Wizara ya Nishati na unatekelezwa katika mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Gharama za mradi ni **shilingi 25,224,256,613.88,** na kati ya kiasi hicho **shilingi 1,547,480,194.89** ni kwa ajili ya wakandarasi washauri na **shilingi 23,676,776,415.9** ni kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi (NHC).

Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 12 Machi, 2024, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 75.09** na kiasi cha **shilingi 16,480,633,639.89** sawa na **asilimia 65.33** ya gharama za mradi kilikuwa kimelipwa kwa wakandarasi wanaotekeleza na kusimamia mradi.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 22 Novemba, 2021 na ulitakiwa kukamilika tarehe 29 Novemba, 2023. Hata hivyo, mradi haukukamilika katika muda huo kutokana na mkandarasi kuchelewa kuwasilisha malighafi za ujenzi kutoka nje ya nchi. Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kuchelewa huko ni uhaba wa fedha za kigeni (dola za marekani). Sababu hiyo ilifanya muda wa mkataba kurefushwa kwa miezi sita (6) na sasa unatarajiwa kukamilika ifikapo 29 Mei, 2024 baada ya changamoto ya uhaba wa dola za kimarekani kutatuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea mradi huu na kuangalia utekelezaji wake ilibaini kasi ndogo ya utekelezaji wake na hivyo kuleta mashaka iwapo utekekelezaji wake utakamilika kwa wakati ikilinganishwa na muda wa takribani miezi mitatu iliyobaki. **Ni ushauri wa Kamati kwamba, Wizara iimarishe usimamizi ili kuhakikisha mradi unakamilika ndani ya muda wa mkataba na jengo hilo kutoa huduma inayokusudiwa**.

### 2.1.2 Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Lemugur (Na. 3175), Kisongo-Arusha

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki ni sehemu ya nne (Lot 4) kati ya sehemu sita (six lots) za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia yenye urefu wa kilomita **414.3** ya kusafirisha umeme wa msongo wa **Kv 400** kutoka Singida hadi Namanga. Kwa ujumla utekelezaji wa sehemu zote sita za mradi unagharimu Dola za Marekani **milioni 258.82**, kati ya hizo **asilimia 83** zinatolewa na wafadhili AfDB na JICA na **asilimia 17** Serikali ya Tanzania.

Ujenzi wa Kituo hiki unahusu upanuzi wa kituo cha kupoza umeme (substation) cha Lemugur, Arusha na unagharimu Dola za Marekani **milioni 36** na hadi kufikia mwezi Machi, 2024 utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 99.27** na sasa mradi upo katika hatua ya majaribio.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mafanikio ya awali kutokana na ujenzi wa kituo hiki ni pamoja na kuiwezesha TANESCO kuanza mradi wa ujenzi wa njia nane (8) za kusambaza umeme msongo wa **Kv 33.** Lengo la mradi huo ni kukipunguzia mzigo kituo cha kupoza umeme cha Njiro kutokana ongezeko la wateja katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Gharama za mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika Agosti, 2024 ni Dola za Marekani **Milioni 1.56** na shilingi **14,295,364,097.20** ambazo zinatolewa na Serikali ya Tanzania. Wakati Kamati inatembelea mradi huu, utekelezaji ambao ulianza Machi, 2023 ulikuwa umefikia **asilimia 35**. **Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kuboresha huduma ya ugavi katika maeneo yanayohudumiwa na kituo cha Njiro**.

**Mheshimiwa Spika,** faida nyingine za utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na:-

(a) Kuwezesha Tanzania kuunganishwa na umeme wa pamoja wa upande wa mashariki mwa Afrika (East African Power Pool-EAPP) na hivyo kuingia katika biashara ya nishati na nchi nyingine; na

(b) Kuimarisha uwezo wa usambazaji wa umeme katika nchi za Kenya, Tanzania na eneo la mashariki mwa Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi wa mradi huu, Kamati ilipata taarifa kuhusu utekelezaji wa sehemu ya tano (Lot 5) ambayo ilihusu usambazaji wa umeme katika vijiji kumi na tisa (19) vilivyopitiwa na mradi kwa gharama ya Dola za Marekani **Milioni 4.4.** Mradi umekamilika na jumla ya **wateja 10,000** walikusudiwa kunufaika na mradi huu kwa kuunganisha umeme. Hata hivyo ilibainika kuwa ni **wateja 608** sawa na **asilimia 6.08 tu** ndio waliokuwa wameunganishwa.

### 2.1.3 Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kujaza gesi asilia kwenye magari (CNG) (Na. 3162), Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua vituo vikuu (CNG mother stations) viwili vya kujaza gesi asilia kwenye magari ambavyo viko Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Kipawa na Ubungo, katika mkoa wa Dar es Salaam. Uchambuzi kuhusu ukaguzi wa kila kituo ni kama ifuatavyo: -

#### (a) Kituo cha TAQA-*Dalbit* kilichopo Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Kipawa, Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki kilianza kazi tarehe 11 Novemba, 2023 na kina pampu sita zenye uwezo wa kuhudumia magari sita kwa wakati mmoja. Ni miongoni mwa vituo mama (mother CNG stations) kwa kuwa kinapokea gesi asilia moja kwa moja kutoka kwenye bomba lililojengwa na kampuni ya *PanAfrican Energy Tanzania Ltd* (PAET) kwa kushirikiana na TPDC. Aidha, kituo

hiki kina karakana ya kuweka mfumo wa kutumia gesi kwenye magari ambayo yameingizwa nchini yakiwa hayana mfumo huo.

Kamati ilifahamishwa kuwa, kituo hiki chenye uwezo wa kujaza gesi asilia takribani **magari 1000** kwa siku kinafanya kazi saa 24 jambo linalosaidia kupunguza msongamano na hivyo kuwawezesha wateja kutumia muda mfupi kwenye kupata huduma. Wakati wa ukaguzi, kamati ilishuhudia ufanyaji kazi wa mfumo wa kuigandamiza gesi inayopokelewa kutoka kwenye bomba ili iweze kutumika kwa ajili ya magari, uwekaji wa mfumo wa gesi kwenye magari na ujazaji wa gesi kwenye magari kwa kuhudumia idadi kubwa ya wateja bila ya kusababisha msongamano.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ufanisi ulioshuhudiwa na kamati katika uendeshaji wa kituo hiki, zipo changamoto kadhaa zinazokikabili kituo hiki ikiwa ni pamoja na kituo kutegemea nishati ya umeme pekee kujiendesha. Hali hii inasababisha kukosekana kwa huduma ya kujaza gesi kwenye magari mara umeme unapokatika. **Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali itoe kipaumbele katika upatikanaji wa umeme kwenye maeneo yanayotoa huduma ya kujaza gesi kwenye magari, ili kuwawezesha wamiliki wa vituo hivyo kutoa huduma muda wote, hasa ikizingatiwa**

**kwamba utumiaji wa kangavuke (*generator*) unaweza kusababisha gharama za kujaza gesi kuwa kubwa**.

**(b) Kituo cha PAET/TPDC kilichopo Ubungo, Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki ni miongoni mwa vituo mama (CNG mother stations) vya kujaza gesi kwenye magari na kinamilikiwa kwa ubia baina ya TPDC na Kampuni ya PAET. Kituo hiki kinachofanya kazi saa 24 kutokana na pampu mbili zilizopo, kina uwezo wa kuhudumia wastani wa magari 750 kwa siku.

Kutokana na eneo kilipo kituo hiki, wateja wengi huvutiwa kujaza gesi hapo, jambo linalosababisha msongamano mkubwa wa magari yanayosubiri kujaza gesi hasa nyakati za asubuhi na mchana. Aidha, kamati ilijulishwa kuwa idadi ya watumiaji wa gesi kwenye magari imekuwa ikiongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta.

Kamati ilipohoji kuhusu uwezekano wa kuongeza pampu ili kukabili msongamano, ilijulishwa kwamba suala hilo haliwezekani kutokana na ufinyu au udogo wa eneo la kituo. **Baada ya uchambuzi, Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha inatatua tatizo la foleni katika eneo hilo ndani ya muda mfupi ikiwemo ujenzi wa vituo vingine hatua ambayo itasaidia kuhamasisha watu wengi kujiunga na matumizi ya gesi asilia kwenye magari**.

### 2.1.4 Mradi wa ujenzi bomba la kusafirisha gesi asilia kwa ajili ya kupikia na viwandani (Na. 3162), Mwenge-Mbezi Beach, Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua ujenzi wa bomba kutokea Mwenge hadi Afrikana, Mbezi beach na viwanda vinavyotumia gesi asilia kuendeshea mitambo. Ujenzi wa bomba hilo umekamilika na tayari wateja wameomba kuunganishiwa huduma hiyo hususani baadhi ya viwanda na hoteli ambao wameanza kuandaa miundombinu itakayowawezesha kutumia gesi asilia.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa wateja wanaotumia gesi asilia kuendeshea mitambo ni kiwanda cha mabati cha **Kiboko** na kiwanda cha kuzalisha karatasi laini na vifungashio cha **TanPack Tissue Ltd** vilivyopo Mikocheni, Dar es Salaam. Gesi inayotumika katika viwanda hivi inatokana na bomba lililojengwa kwa ubia baina ya TPDC na Kampuni ya PAET. Kamati ilijulishwa kuwa matumizi ya gesi kwenye viwanda hivyo ni nafuu zaidi kwa wastani wa **asilimia 25** ikilinganishwa na matumizi ya umeme na mafuta.

Pamoja na unafuu huo wa matumizi ya gesi, wamiliki wa viwanda hivyo walilalamika kununua gesi hiyo kwa bei ya juu ikilinganishwa na bei wanayotozwa wamiliki wa viwanda vingine vinavyotumia nishati hiyo. Ilielezwa kwamba, wakati viwanda hivyo vinanunua *unit* moja ya gesi kwa kiasi cha Dola za Marekani **9.3**, viwanda vingine vinanunua *unit* hiyo kwa

Dola za Marekani **6.7**. Kamati ilipohoji juu ya tofauti hiyo ya bei, ilijulishwa kwamba viwanda hivyo vinauziwa gesi na Kampuni ya PAET ambayo bei yake iko juu ikilinganishwa na gesi inayouzwa na TPDC. **Ni maoni ya Kamati kwamba Serikali iangalie namna ya kuwianisha bei ya gesi asilia kwa wateja wote ili kuondoa malalamiko na kuweka mazingira sawa ya kibiashara**.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu gharama za nishati mbalimbali za kupikia umebaini kwamba, matumizi ya gesi asilia (LNG) ni nafuu zaidi ikilinganishwa na matumizi ya nishati nyingine. Kielelezo Na.1kinafafanua zaidi.

**Kielelezo Na. 1:** Ulinganisho wa bei za nishati mbalimbali katika kupikia

| Nishati ya Kupikia | Tshs/MMbtu | Kuokoa Gharama |
|---|---|---|
| Gesi asilia (LNG) | 27,738.09 | Benchmark |
| Mkaa | 40,523.41 | 32% |
| Gesi ya Mitungi (LPG) | 76,670.40 | 64% |
| Umeme | 105,420.60 | 74% |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Wizara ya Nishati na Usanifu wa Kamati*

### 2.1.5 Mradi wa Umeme Vijijini (REA) (Na. 3113) Halmashauri ya Chalinze, Bagamoyo, Mkoa wa Pwani

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ufungaji wa mashine umba **22** na kupeleka umeme kwenye **vijiji 22** ambavyo vilikuwa havijafikiwa katika halmashauri ya Chalinze. Gharama za mradi ni **shilingi 7,827,305,757** na utekelezaji

wake ulianza Agosti, 2021 na kukamilika Machi, 2024. Mradi ulikusudiwa kufikishia umeme wateja **1,452,** hata hivyo wakati Kamati inatembelea mradi huu, ni wateja **1,236** ndiyo walikuwa wameunganishiwa umeme kwenye nyumba zao sawa na **asilimia 85** ya lengo. Kwa upande wa uunganishaji wa umeme kwenye taasisi za umma zikiwemo shule, hospitali, misikiti na makanisa, utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 91**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujiridhisha na hali halisi ya huduma ya umeme vijijini, Kamati ilitembelea Kijiji cha Tukamisasa ambacho ni cha mwisho kufikiwa na huduma ya umeme kwa gharama ya **shilingi Milioni 466**. Kamati ilielezwa kuwa, umeme katika Kijiji hicho una wigo wa wateja wa **awali 64**, lakini hadi wakati wa ukaguzi ni **wateja 23** tu ndio walikuwa wameunganishwa.

Kamati ilipohoji kuhusu idadi ndogo ya wateja kuunganishiwa umeme sababu mbalimbali zilitolewa kama ifuatavyo:

(a) Uhamasishaji hafifu kutoka kwa viongozi kutokana na uwepo wa taarifa kuwa mradi wa REA ambao ndio unaolipiwa **shilingi 27,000** umefikia ukomo na umebaki mradi wa TANESCO ambao gharama yake ni zaidi ya **shilingi 300,000**;

(b) Umeme kutokufika kwenye vitongoji vilivyo nje ya barabara zilizojengwa miundominu ya umeme;

(c) Kaya nyingi kutokuandaa miundombinu ya kupokelea umeme kwenye nyumba zao; na

(d) Ukosefu wa mashine umba (transfoma) katika baadhi ya vitongoji licha ya kupitiwa na miundombinu ya umeme.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa sababu zilizoelezwa katika halmashauri ya Chalinze hususani kijiji cha Tukamisasa kwa watu wengi kutokuunganisha umeme kwenye nyumba zao licha ya umeme kufika katika vijiji vyao, kwa sehemu kubwa ndizo changamoto zilizoko katika vijiji vingi nchini.

Wakala wa Umeme Vijijini (REA) pia unatekeleza mradi wa kupeleka umeme kwenye migodi midogo na maeneo ya kilimo kwenye jumla ya maeneo kumi na nne (14) katika wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya **wateja tarajiwa 78**. Mradi huo utakaogharimu **shilingi 2,456,801,235.70** ulianza kutekelezwa Machi, 2023 na unategemewa kukamilika Septemba, 2024. Hadi wakati wa ukaguzi, maeneo manne **(4)** tu sawa na **asilimia 28** ya lengo ndio yalikuwa yamepata huduma ya umeme.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele kumi na nne **(14).** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa sehemu kubwa Wizara imetekeza vipaumbele hivyo kwa kiasi cha kuridhisha. Aidha, utekelezaji wa baadhi ya vipaumbele haukuwa wa kuridhisha.

Miongoni mwa vipaumbele vilivyotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha ni ujenzi wa miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo mradi wa Julius Nyerere (JNHPP-**MW2,115**) ambao hadi Februari, 2024 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 96**, mradi wa kuzalisha umeme Rusumo **MW 26.67** ambao umekamilika na mradi wa kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme wa gesi asilia katika kituo cha kinyerezi I extension **MW 185** ambao pia umekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa vipaumbele ambavyo utekelezaji wake haukuwa wa kuridhisha, Kamati imetoa ushauri kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wake kufanyika kadri ulivyopangwa. Vipaumbele hivyo ni pamoja na: -

(a) Kupeleka umeme katika vitongoji **36,336** sawa na **asilimia 56** ya vitongoji **64,760** vya Tanzania bara. Hadi Februari, 2024 utekelezaji wa kipaumbele hiki ni **asilimia 10.2** ambapo kazi zilizofanyika ni ununuzi wa vifaa na kusimika nguzo katika mkoa wa Songwe na Kigoma kwa lengo la kufikisha umeme kwenye **vitongoji 654.** Aidha, tathmini kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa kutekeleza mradi huu katika **vitongoji 3,060** imekamilika.

(b) Kuhakikisha upatikanaji wa umeme nchini kupitia mradi wa kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization) ambapo kazi zilizofanyika ni kukamilisha taratibu za kuwapata wakandarasi na kusainiwa kwa mikataba ya miradi yote ya gridi imara, ukaguzi wa njia za kusafirishia

umeme, upembuzi yakinifu wa njia za kusafirishia umeme, usanifu wa michoro, ununuzi wa vifaa kwa baadhi ya miradi pamoja na kuanza kazi za ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa sababu za kutokutekelezwa ipasavyo kwa kipaumbele hiki ni pamoja na kutolewa kwa kiasi kidogo cha fedha kwani hadi Februari, 2024, ni **shilingi Bilioni 132.6** tu kati ya **shilingi Bilioni 473.4** zilizotengwa sawa na utekelezaji wa asilimia **28.02**.

## 2.3 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2024

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya **Shilingi 20,392,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 9,942,015** sawa na **asilimia 49** ya lengo. Kielelezo Na. 2 kinafafanua.

**Kielelezo Na. 2: Makusanyo ya Maduhuli hadi Februari, 2024**

| Chanzo cha Mapato | Kiasi kilichopangwa | Kiasi kilichokusanywa | Asilimia ya lengo |
|---|---|---|---|
| Stakabadhi nyinginezo | 1,000 | 0 | 0 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 20,391,000 | 9,942,015 | 49 |
| Stakabadhi za aina mbalimbali | 1,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **20,393,000** | **9,942,015** | **49** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara hii ulikuwa chini ya lengo. Hata hivyo, ilielezwa kuwa hali hiyo imesababishwa na Wizara kutegemea kwa asilimia kubwa (99.9%) makusanyo kutoka chanzo kimoja ambacho ni urejeshaji wa masurufu (*imprest*). **Ni mtazamo wa Kamati kwamba Wizara ibuni vyanzo vipya vya mapato**.

### 2.4 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2024

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Nishati (**Fungu 58**)iliidhinishiwa na Bunge **Shilingi 3,048,632,519,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya

matumizi ya kawaida ni **Shilingi 87,929,698,000.00** sawa na **asilimia 2.9** ya fedha yote ambapo **Shilingi 16,292,586,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (P.E) na **Shilingi 71,637,112,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa **Shilingi 2,960,702,821,000.00** sawa na **asilimia 97.1** ya bajeti yote ambazo zinajumuisha fedha za ndani **Shilingi 2,609,156,128,000.00** na fedha za nje **Shilingi 351,546,693,000.00**

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 1,310,852,090,180.49** sawa na **asilimia 52.27** ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 24,089,029,668.19** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **shilingi 11,386,327,902.48** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **Shilingi 12,702,701,765.71** sawa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, zilipokelewa **shilingi 1,569,534,870,633.73** sawa na **asilimia 53.42** ya kiasi kilichotengwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,324,485,523,330.90** ni fedha za ndani na **Shilingi 245,049,347,302.73** ni fedha za nje. Mchanganuo wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.3**.

**Kielelezo Na. 3:** Upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa kipindi cha Julai, 2023 - Februari, 2024

| Aina | Kilichoidhinishwa | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | **16,292,586,000** | **11,386,327,902.48** | **69.88** |
| **Oc** | **71,637,112,000** | **12,702,701,765.71** | **17.73** |
| **Maendeleo Ndani** | **2,609,156,128,000** | **,324,485,523,330.90** | **50.76** |
| **Maendeleo Nje** | **351,546,693,000** | **245,049,347,302.73** | **69.70** |
| **JUMLA** | **3,048,632,519,000** | **1,310,852,090,180.49** | **52.27** |

***Chanzo***: *Taarifa ya utekelezaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umebaini kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) haukuwa wa kuridhisha. Kamati ilipohoji kuhusu hali hiyo ilielezwa kuwa ilisababishwa na kutokupokelewa kwa fedha za IMF kutoka nje jumla ya **shilingi Bilioni 53.2. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ihakikishe inafuatilia upatikanaji wa fedha hizo ili kutoendelea kuathiri mipango iliyokusudiwa kutekelezwa.**

## 2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliyowasilishwa Bungeni mwezi Mei, 2023 pamoja na mambo mengine, ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo yapatayo 24 ili yafanyiwe kazi na Wizara.

Katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 20 Machi, 2024, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Tathmini inaonesha kuwa, Wizara imetekeleza ushauri na mapendekezo yaliyotolewa kwa kiwango cha kuridhisha isipokuwa kwa baadhi ya hoja chache zifuatazo: -

(a) TANESCO kulipa deni lote inalodaiwa na TPDC kiasi cha **shilingi Bilioni 720** katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hoja hii haikutekelezwa kutokana na mapato ya TANESCO kuwa kidogo ikilinganishwa na mahitaji. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, kutokulipwa kwa fedha hizi kunaathiri uwezo wa TPDC katika kutekeleza kikamilifu shughuli zake ikiwa ni pamoja na miradi ya uzalishaji wa gesi asilia ambayo ni muhimu pia kwa ajili ya TANESCO katika kuzalisha umeme; na

(b) Taasisi zote zinazodaiwa na TANESCO ankara za umeme jumla ya **shilingi Bilioni 334.8** kulipa madeni yote katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hadi Februari, 2024 deni

linalodaiwa na TANESCO ni **shilingi Bilioni 86.3.** Kamati ilielezwa kuwa, madeni haya yanatokana na taasisi zinazotumia mita za umeme za zamani kutokana na kuwa na matumizi makubwa ya umeme ambayo hayawezi kutumia mita za LUKU kama ilivyo kwenye nyumba za makazi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokulipwa kwa madeni haya kikamilifu kunaathiri utendaji wa TANESCO na kuipunguzia uwezo wa kutekeleza miradi yake. Ni msisitizo wa Kamati kuwa, Serikali isimamie na kuhakikisha taasisi zinazodaiwa na TANESCO zinalipa madeni stahiki kwani zinaidhinishiwa katika bajeti fedha za kununua umeme.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

a) Uchambuzi wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
b) Uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
c) Uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
d) Ulinganisho kati ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025; na
e) Uchambuzi wa masuala mahsusi ya kisekta.

### 3.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umebaini kuwa, malengo na vipaumbele vya Wizara vimezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 –

2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati wa Mwaka 2021/2022-2025/2026.

Ili kufikia malengo ambayo yamefafanuliwa kwa kina kupitia mpango mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/2022-2025/2026, Wizara inakusudiwa kutekeleza jumla ya vipaumbele tisa (9). Baadhi ya vipaumbele hivyo ni: -

a) Kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia;

b) Kuendelea kupeleka nishati vijijini, ikiwemo kusambaza umeme katika vitongoji vya Tanzania Bara, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa nishati ya mafuta vijijini kupitia uanzishwaji wa vituo vya mafuta;

c) Kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwa ni pamoja na mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (*Liquefied Natural Gas-LNG Project*) na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline -EACOP*);

d) Kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati pamoja na kusambaza gesi asilia viwandani, taasisi, makazi na magari;

e) Kuendelea kuimarisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia (clean cooking) nchini; na

f) Kuendelea kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya vipaumbele vya mwaka wa fedha 2024/2025 vilikuwepo katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, vipaumbele vya mwaka wa fedha 2024/2025 vimepungua kutoka kumi na nne (14) hadi tisa (9) kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pomoja na baadhi ya miradi kukamilika na kupungua kwa bajeti ya Wizara kwa asilimia 38 ikilinganishwa na mwaka unaoisha.

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **shilingi 8,000,000.00** kutoka kwenye vyanzo vyake viwili. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya ni pungufu kwa kiasi cha **shilingi 12,392,000** sawa na **asilimia 60.8** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo yalikuwa **shilingi 20,392,000.00**.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Wizara imezingatia ushauri uliowahi kutolewa na Kamati katika mwaka wa fedha 2022/2023 uliohusu makadirio ya makusanyo ya

maduhuli kuendana na uhalisia. Kielelezo Na. 4 kinaeleza kuhusu ulinganisho wa maduhuli.

**Kielelezo Na. 4: U**linganisho wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025

| CHANZO | 2023/2024 | 2024/2025 | ONGEZEKO /UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Marejesho ya Fedha za Umma (Recovery of Public Money) | **20,391,000** | **7,999,000** | **12,392,000** | **60.8** |
| Stakabadhi nyinginezo | **1,000** | **1,000** | **0** | **0** |
| Stakabadhi za aina mbalimbali | **1,000** | **-** | **-** | **-** |
| **JUMLA** | **20,393,000** | **8,000,000** | **12,392,000** | **60.8** |

***Chanzo**: Randama ya Wizara ya makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na usanifu wa Kamati*

## 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Nishati inaomba kuidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,883,759,455,000.00**. Fedha hizi zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 88,892,623,000/=** sawa na **asilimia 4.7** ya bajeti yote ya Wizara. Katika fedha hizo, **shilingi 19,368,422,000.00** ni kwa ajili ya mishara (PE) na **shilingi 69,524,201,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Kamati ilielezwa kuwa, katika fedha za matumizi mengineyo (OC), kiasi cha **shilingi 53,200,000,000.00** ni fedha za nje (IMF) kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) pamoja na kutekeleza miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa na umeme vijijini (REA-HEP).

Aidha, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ni shilingi **1,794,866,832,000.00** sawa na **asilimia 95.3** ya bajeti yote ya Wizara, ambapo **shilingi 1,536,020,274,000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 258,846,558,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kwa kiasi cha **shilingi 1,164,873,084,000.00** sawa na **asilimia 38.21** ikilinganishwa na bajeti ya Wizara hii ya mwaka wa fedha 2023/2024. Kielelezo Na.5 kinafafanua ulinganisho huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kutokana na kupungua kwa ukomo wa bajeti (Budget ceiling) iliyotolewa na Serikali ikilinganishwa na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo ukomo wa bajeti ulikuwa juu. Vilevile, kupungua kwa bajeti katika mwaka ujao wa fedha kunahusianishwa na kukamilika kwa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao bajeti yake ilikuwa **shilingi 1,500,000,000,000.00** sawa na **asilimia 51.72** ya bajeti yote ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara.

**Kielelezo Na. 5:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025

| WIZARA YA NISHATI - FUNGU 58 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2023/2024** | **2024/2025** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **ASILIMIA** |
| **Maendeleo** | Fedha za Ndani | 2,609,156,128,000 | 1,536,020,274,000 | 1,073,135,854,000 | 41.13 |
| | Fedha za Nje | 351,546,693,000 | 258,846,558,000 | 92,700,135,000 | 26.37 |
| | **Jumla ndogo** | **2,960,702,821,000** | **1,794,866,832,000** | **1,165,835,989,000** | **39.38** |
| **Matumizi ya kawaida** | Mengine yo (OC) | 71,637,112,000 | 69,524,201,000 | 2,112,911,000 | 2.95 |
| | Mishahara (PE) | 16,292,586,000 | 19,368,422,000 | 3,075,836,000 | 18.88 |
| | **Jumla ndogo** | **87,929,698,000** | **88,892,623,000** | **962,925,000** | **1.1** |
| **JUMLA KUU** | | **3,048,632,519,000** | **1,883,759,455,000** | **1,164,873,064,000** | **38.21** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Wizara kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 na Usanifu wa Kamati*

## 3.4 Ulinganisho baina ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulienda mbali zaidi kwa kulinganisha Bajeti ya Wizara hii na Bajeti ya Taifa. Ulinganisho huo uliangalia bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambayo ni **shilingi 3,048,632,519,000** na bajeti ya 2024/2025 ambayo ni **shilingi 1,883,759,455,000** dhidi ya bajeti ya Taifa kwa kipindi hicho ambayo ni **shilingi 44,388,100,000,000** mwaka 2023/2024 na **shilingi 49,345,700,000,000** mwaka 2024/2025. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali yafuatayo: -

a) Bajeti ya Wizara kwa ujumla dhidi ya Bajeti ya Taifa imeshuka kutoka **asilimia 6.87** mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 3.8** kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

b) Katika upande wa matumizi mengineyo, bajeti ya Wizara imeshuka kutoka **asilimia 0.66** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 0.26** mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na bajeti ya Taifa.

c) Katika bajeti ya maendeleo, fedha za ndani za Wizara zimepungua kutoka **asilimia 21.97** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 12.64** mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na bajeti ya Taifa.

d) Katika bajeti ya maendeleo, fedha za nje zimepungua kutoka **asilimia 10.71** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **asilimia 7.11** mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti ya Wizara imepungua katika nyanja zote ilihali bajeti ya Taifa imeongezeka.

**Kielelezo Na. 6:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

| BAJETI YA TAIFA DHIDI YA BAJETI YA WIZARA MWAKA 2024/2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI YA TAIFA** | **BAJETI YA NISHATI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 33,556,600,000,000 | 1,794,866,832,000 | 5.35 |
| **Mishahara** | 11,997,800,000,000 | 19,368,422,000 | 0.16 |
| **Maendeleo ndani** | 12,148,300,000,000 | 1,536,020,274,000 | 12.64 |
| **Maendeleo nje** | 3,640,800,000,000 | 258,846,558,000 | 7.11 |
| **Deni la Serikali** | 15,746,700,000,000 | - | - |
| **JUMLA KUU** | **49,345,700,000,000** | **1,883,759,455,000** | **3.8** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Randama ya Wizara ya Nishati mwaka wa fedha 2024/2025 na Usanifu wa Kamati.*

## 3.5 Uchambuzi wa Masuala Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi wa bajeti, Kamati imejiwekea utaratibu wa kufuatilia masuala mahsusi ya kisekta kwa kuwa yana maslahi kwa wananchi na nchi kwa ujumla. Masuala hayo ni mwenendo wa upatikanaji wa umeme pamoja na mwenendo wa biashara ya mafuta nchini. Uchambuzi kuhusu masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.5.1 Mwenendo wa Upatikanaji wa Umeme

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, hali ya upatikanaji wa umeme nchini imekuwa ikibadilika katika vipindi tofauti. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 hali haikuwa ya kuridhisha na hivyo kusababisha mgao katika sehemu kubwa ya nchi. Katika kipindi cha Januari hadi Aprili,

2024, hali ya upatikanaji wa umeme imeonekana kuimarika na hivyo mgao kupungua.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusiana na mitambo ya kuzalisha umeme, hadi Februari, 2024 uwezo wa mitambo kuzalisha umeme (*installed capacity*) ulikuwa **MW 2,129.85.** Kiwango hiki ni ongezeko la **MW 307.8** ikilinganishwa na uwezo wa mitambo wa **MW 1,822.05** mwezi Februari, 2023. Licha ya uwezo wa mitambo kuwa juu, uzalishaji halisi (production capacity) hadi Februari, 2024 ulikuwa wastani wa **MW 1,756.42** sawa na uwezo wa uzalishaji wa **asilimia 82.5** ikilinganishwa na uwezo wa mitambo iliyosimikwa. Kielelezo Na.7 kinafafanua zaidi.

**Kielelezo Na. 7:** Mchanganuo wa uwezo wa mitambo katika gridi ya Taifa hadi Mwezi Februari, 2024

| **Chanzo** | **Uwezo wa Mitambo (Installed Capacity)** | | **Uzalishaji unaopatikana (Available production)** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **MW** | **Uwezo wa mitambo (%)** | **Chanzo** | **MW** | **Uzalishaji (%)** |
| Maji | 836.61 | 39.3 | Maji | 755.56 | 90.31 |
| Gesi Asilia | 1,198.82 | 56.3 | Gesi Asilia | 935.11 | 78 |
| Mafuta | 83.92 | 3.9 | Mafuta | 65.75 | 78.35 |
| Tungamotaka | 10.5 | 0.5 | Tungamotaka | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2,129.85** | **100** | **Jumla** | **1,756.42** | **82.5** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mitambo iliyopo inazalisha umeme chini ya uwezo wake kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uchakavu wa miundombinu ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme na upungufu wa uzalishaji wa gesi asilia ikilinganishwa na mahitaji ya gesi yaliyopo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya umeme vijijini, hadi Februari, 2024, jumla ya **vijiji 11,837** kati ya **vijiji 12,318** vilivyopo nchini vimefikiwa na huduma ya umeme, sawa na **asilimia 96.1**. Aidha, kwa upande wa vitongoji, hadi kufikia Februari, 2024 asilimia **50.54** (**vitongoji 32,730** kati ya **vitongoji 64,760)** vilivyoko nchini vilikuwa vimefikiwa na huduma ya umeme.

Ili kuhakikisha maeneo yote ya nchi yanapata umeme, Serikali ilianzisha mradi wa umeme maeneo ya pembezoni mwa miji (*peri urban)* ambao utekelezaji wake uko awamu ya Tatu. Awamu hii imepangwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2024. Hata hivyo, utekelezaji wake unasuasua kwani hadi Februari, 2024 ulikuwa umefikia **asimilia 19.8 tu** kwa kufika katika maeneo **83** kati ya **420** yaliyokusudiwa, na kuunganishia umeme wateja **1,166** kati ya **18,426.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la uhitaji wa umeme nchini kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo idadi kubwa ya wananchi wanaosubiri kuunganishiwa umeme hususani maeneo ya vijijini,

pembezoni mwa miji na maeneo ya uzalishaji ikiwemo wachimbaji wadogo na viwanda. **Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kukamilisha miradi ya kuzalisha umeme inayotekelezwa ikiwemo, mradi wa umeme wa jua Shinyanga (MW 150) na Julius Nyerere (JNHPP MW 2115) ili kupunguza upungufu wa umeme katika maeneo yaliyosalia ambayo hayajapata huduma ya umeme.**

3.5.2 **Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu uagizaji wa mafuta nchini kupitia Wakala wa Uagizaji wa mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa kutumia mfumo wa manunuzi ya pamoja (*Bulk Procurement System* – BPS). Uchambuzi wa Kamati kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta unaonesha kuwa, nchi ina akiba ya mafuta inayotosheleza mahitaji. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 akiba ya mafuta nchini ilikuwa **siku 25** ambazo ni juu ya wastani wa mahitaji (**siku 15**). Katika kipindi hicho, jumla ya **Tani 4,453,479** ziliingizwa nchini kupitia zabuni **78** zilizotolewa na PBPA. Kiasi hicho ni ongezeko la **Tani 190,234** za mafuta sawa na **asilimia 4.46** ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 ambapo uagizaji ulikuwa **Tani 4,263,245.**

Katika kiasi hicho kilichoingizwa nchini, Tani **2,228,238** sawa na **asilimia 50.03** ni kwa ajili ya matumizi ya ndani (*local*) na kiasi cha **Tani 2,225,241** sawa na **asilimia 49.97** ni mafuta yanayopita kwenda nchi jirani (*on transit*).

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa na akiba toshelezi ya mafuta nchini, bei ya mafuta iliendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupanda kwa gharama za usafiri na ongezeko la bima ya meli zinazosafirisha mafuta kutokana na vita vya Ukraine na Urusi, uhaba wa Dola za Marekani na kuongezeka kwa gharama za kubadilisha fedha za kigeni *(exchange rate*). **Ni msisitizo wa Kamati kuwa Serikali iendelee na jitihada za kupunguza athari za bei ya mafuta kuwa juu nchini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia kwenye magari**.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huu, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kama ifutavyo:-

### 4.1 Wizara ya Nishati

a) Kutokana na umuhimu wa Jengo la Wizara linalojengwa katika mji wa Serikali mtumba, na kutokana na kasi ya utekelezaji wake kuonekana sio ya kuridhisha, Wizara iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike katika muda ulioongezwa na kwa viwango stahiki.

b) Kutokana na kutokupokelewa kwa fedha za nje **shilingi 53,200,000,000.00** kwa ajili matumizi mengineyo, Wizara ifuatilie na kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kutoathiri utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa.

### 4.2 Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO)

a) Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutokea Singida hadi Namanga ulihusisha kupeleka umeme kwenye vijiji kumi na tisa (19) vilivyopitiwa na mradi huo. Hata hivyo, ni **wateja 608** tu kati ya **10,000** waliokusudiwa ndio wameunganishiwa umeme idadi ambayo ni ndogo sana. Kwa kuwa kumekuwepo na tatizo la aina hii katika maeneo mengi nchini, Serikali ihakikishe TANESCO

inashirikiana na REA kubuni mbinu zitakazoamsha ari ya wananchi na kuhamasisha matumizi ya umeme kwenye shughuli zao;

b) TANESCO iongeze kasi katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ili kuwezesha nchi kuwa na utoshelevu na uhakika wa umeme;

c) TANESCO iongeze kasi ya kutekeleza miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa ili kuondoa changamoto ya kukatika kwa umeme kutokana na uchakavu wa miundombinu, na umeme kupungua nguvu na kupotea kutokana na kusafiri umbali mrefu bila kupozwa;

d) Kwa kuwa nchi imeanza kujitosheleza kwa kiwango na uhakika wa umeme kutokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya kuzalisha umeme (JNHPP, Rusumo na Kinyerezi I Extension), Serikali ihakikishe maeneo ya uzalishaji kama vile migodi, viwanda na skimu za umwagiliaji, yanapata umeme wa kutosha na wa uhakika;

e) Serikali ihakikishe ujenzi wa njia za kusafirishia umeme ambao umepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 unahusisha kuunganisha mikoa iliyosailia kwenye gridi ya Taifa;

f) Mpango wa kuzalisha umeme (**MW 200)** kutokana na makaa ya mawe ya Kiwira, Mbeya ni wa muda mrefu

bila kuanza utekelezaji, jambo linaloikosesha nchi fursa ya kunufaika na rasilimali za asili zilizopo. Serikali ihakikishe utekelezaji wa mradi huu unaanza ili nchi iweze kunufaika na rasilimali hiyo kama ilivyo katika nchi nyingine zenye rasilimali ya aina hii;

g) Serikali iongeze kasi ya uhamasishaji, uwezeshaji na utekelezaji wa mradi wa nishati safi ya kupikia kwa kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa utoshelevu na bei nafuu; na

h) Mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia tungamotaka ya mabaki ya miwa nchini ina uwezo wa kuzalisha **MW 10.5.** Hata hivyo, mitambo hiyo haifanyi kazi kikamilifu kutokana na kutegemea mabaki ya miwa tu ingawa inaweza kutumia tungamotaka nyingine. Serikali ihakikishe mitambo hiyo inazalisha umeme kwa kutumia tungamotaka za aina mbalimbali kama vile taka laini zinazozalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

### 4.3 Wakala wa Umeme Vijijini –REA

a) Ili kuondoa tofauti ya gharama za kuunganishiwa umeme katika vijiji ambapo baadhi hulipa shilingi 27,000.00 na wengine zaidi ya shilingi 300,000.00 (mfano kijiji cha Tukamisasa, Chalinze-Bagamoyo), jambo linaloleta malalamiko miongoni mwa wananchi, Serikali

ifanye mapitio ili kuwianisha gharama hizo na hivyo kuondoa malalamiko yaliyopo;

b) Serikali iongeze kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 32,030 vilivyosalia (ambavyo ni asilimia 49.5 ya vitongoji vyote nchini) Ili kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kupata na kunufaika na nishati ya umeme nchini kama ilivyo kwa maeneo yenye huduma ya umeme; na

c) Utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme pembezoni mwa miji (peri urban) awamu ya tatu unasuasua licha ya kubakiza muda mfupi (miezi nane) kukamilika. Hadi Februari, 2024 mradi huo ulikuwa umefikisha umeme kwenye **maeneo 83** kati ya **420**, sawa na **asilimia 19.8** ya lengo na hivyo kuibua malalamiko miongoni mwa maeneo ambayo hayajafikiwa. Ili kuondoa malalamiko hayo, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu.

### 4.4 Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC)

a) Usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na kwenye taasisi kwa ajili ya kupikia na kuendeshea mitambo na magari unasuasua. Hivyo basi, TPDC iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kuongeza uzalishaji viwandani, kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia na matumizi ya gesi asilia kwenye magari;

b) Uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi asilia unaelezwa kupungua kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa gesi asilia na kuongezeka kwa matumizi ya gesi hiyo kwenye maeneo mengine. Ili kuondokana na athari hizo, Serikali iongeze uzalishaji kwenye vitalu vilivyopo na ianze uzalishaji katika vitalu vipya kama vile kitalu cha Ruvuma; na

c) Serikali ihakikishe Kampuni Tanzu ya TPDC ya TANOIL inaongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni chechefu yaliyobakia (shilingi bilioni 21) kutoka kwa wadaiwa sugu na kuhakikisha haizalishi madeni mengine yasiyolipika.

## 4.5 Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli – PURA

a) Serikali iharakishe mchakato wa kunadi vitalu vya gesi vilivyo wazi maeneo ya nchi kavu na baharini katika duru ya tano ili kuongeza uzalishaji wa gesi hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji ya gesi nchini yameongezeka kuzidi kiwango cha uzalishaji; na

b) Kwa kuwa zoezi la kutayarisha miongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR) katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia nchini linatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024, Serikali ihakikishe PURA inatoa elimu ya kutosha kuhusu muongozo huo kwa wadau ili kurahisisha utekelezaji wake.

## 4.6 **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

a) Uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta unaofanywa kwa kutumia njia ya mkono umeonesha kutokuwa na vipimo sahihi jambo linalozua manung`uniko miongoni mwa wafanyabiashara ya mafuta kwa kudai kuwa wanapigwa faini ukaguzi unapofanyika. Ili kuondokana na malalamiko hayo na kuleta ufanisi kwenye uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta, Serikali ianzishe uwekaji wa vinasaba kwa njia za kielekroniki;

b) Uwepo wa bei tofauti za gesi asilia miongoni mwa viwanda vinavyotumia gesi katika uzalishaji umesababisha malalamiko miongoni mwa watumiaji hao. Kwa kuwa jukumu mojawapo la EWURA ni kupanga bei ya gesi ili kuweka usawa miongoni mwa watumiaji, Serikali ihakikishe taasisi hiyo inatekeleza jukumu lake kama ilivyo kwenye mafuta, maji na umeme; na

c) Ongezeko la uuzaji holela wa mafuta ya dizeli na petroli maeneo ya vijijini unahatarisha usalama wa raia na mali zao. Serikali ihakikishe EWURA inaimarisha usimamizi wa biashara ya mafuta katika maeneo hayo ili kuepusha uwezekano wa kutokea majanga ya moto.

## 4.7 **Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)**

a) Mfumo wa kudhibiti upotevu wa mafuta (SCADA) unaomilikiwa na PBPA una changamoto ya kutokuonesha mtiririko wa mafuta baada ya kupakuliwa kutoka kwenye meli. Hali hiyo inasababisha mamlaka husika kushindwa kubaini upotevu wa mafuta unaotokea wakati yanasafirishwa kwa njia ya bomba. Ili kudhibiti hali hiyo, Serikali iboreshe mfumo huo na kuuwezesha kuonesha mwenendo wa mtiririko wa mafuta na upotevu unaoweza kutokea wakati wa usafirishaji kwa njia ya bomba;

b) Uhaba wa maghala ya kuhifadhia mafuta nchini ikiwemo mafuta ya ndani na mafuta kwa ajili ya kupeleka nchi jirani (on transit) unaifanya nchi kukosa uhakika na usalama wa hifadhi ya mafuta na hivyo kuchangia kupanda kwa bei mara kwa mara. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuanzisha mradi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (Strategic Petroleum Reserve-SPR) ili kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo, inashauri kasi ya utekelezaji iongezeke ili kuwezesha nchi kuwa na uhakika na usalama wa mafuta; na

c) Uzio wa eneo la *flow meters* zilizopo Kigamboni, Dar es Salaam umezungukwa na makazi binafsi, jambo ambalo linahatarisha usalama wa bomba la mafuta. Aidha, siku za nyuma uliripotiwa wizi wa mafuta kutoka

kwenye bomba uliohusishwa na makazi binafsi. Ili kuepuka kujirudia kwa tatizo la wizi na hujuma kwenye bomba la mafuta, Serikali iangalie uwezekano wa kutwaa maeneo yenye makazi binafsi kuzunguka bomba na *flow meters*.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo: -

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naendelea kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika kuendesha vikao vya Bunge.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano mkubwa wananipatia mimi pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb) ambao umetuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu ya Kamati kwa ufanisi. Kwa namna ya pekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*hansard*) kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb - **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Sophia Hezron Mwakagenda, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. John Marko Sallu, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Martha Festo Mariki, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru Mhe. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa ushirikiano anaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, natoa shukrani zangu kwa Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb), Naibu Waziri wa Nishati, kwa anavyoshirikiana na Kamati na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felschesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu Dkt. James Mataragio kwa namna

wanavyowaongoza watendaji wa Wizara na Taasisi zake na hivyo kurahisisha utendaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc*) pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya Kikatiba.

## 5.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati (**Fungu 58)** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

24 Aprili, 2024